

Maswali kuhusu likizo likizo ya ugonjwa yenye malipo na Coronavirus (COVID-19)

- 1. Je, wafanyakazi wanaweza kutumia likizo ya ugonjwa yenye malipo ili kuficha kutokuwepo kazini iwapo afisa wa umma atafunga mahali pa biashara kuhusiana na COVID-19 Itakuwaje ikiwa mwajiri bado anaendelea na kazi, lakini ana vizuizi vya utendakazi kwa sababu ya amri ya governor?**

Iwapo bado wameajiriwa, wafanyakazi wanawezatumia likizo ya ugonjwa yenye malipo zilizoongezeka. Iwapo mwajiri atamfuta yeyote kazi, mfanyakazi huyo anaweza kutuma ombi la manufaa ya wasioajiriwa.
- 2. Je, wafanyakazi watajuaje iwapo bado wameajiriwa?**

Waajiri lazima wajuliche mfanyakazi iwapo watawafuta kazi. Wafanyakazi wanaweza kutuma ombi la manufaa ya wasioajiriwa iwapo watafutwa kazi au saa zao zimepunguzwa.
- 3. Iwapo shule au mahali pa utunzaji pa motto wa mfanyakazi patafungwa kwa muda kwa sababu ya wasiwasi wa afya, je, mfanyakazi huyo anaweza kutumia likizo ya ugonjwa yenye malipo zilizoongezeka kumtunza mtoto wake?**

Ndio.
- 4. Iwapo mahali pa kazi pa mfanyakazi au shule ya motto imefungwa, je, mwajiri anaweza kukataa ombi la likizo ya ugonjwa na kuhitaji wafanyakazi kufanya kazi wakiwa nyumbani badala yake?**

La.
- 5. Iwapo mwajiri atachagua kufunga mahali pake pa kazi ili kupunguza hatari ya maambukizi ya COVID-19, je mfanyakazi anaweza kutumia likizo ya ugonjwa yenye malipo ili kuficha kutokuwepo kazini?**

Mwajiri halazimiki kuwaruhusu wafanyakazi kutumia likizo ya ugonjwa yenye malipo iwapo biashara yenyewe itaamua kufunga kwa muda kwa sababu ya COVID-19. Aidha, mwajiri anawezaruhusu matumizi ya likizo ya ugonjwa ya muda katika hali hii
- 6. Je, waajiri wanaweza kuwahitaji wafanyakazi waondoke kazi kwa sababu ya hatari ya maambukizi ya COVID-19?**

Mwajiri anaweza kuwahitaji waajiriwa kuondoka kazini. Aidha, waajiri **hawawezi kuwahitaji** waajiriwa kutumia likizo ya ugonjwa yenye malipo ili kuficha kutokuwepo kazini.
- 7. Je, mfanyakazi anayehitajika kuondoka kazini kwa sababu anawezakuwa ameambukizwa COVID-19 anaweza kutumia likizo ya ugonjwa yenye malipo anapokuwa hako kazini?**

Mafanyakazi anaweza kutumia likizo ya muda yenye malipo zilizoongezeka. Aidha, mwajiri hawezi kumlazimisha mfanyakazi kutumia likizo ya muda yene malipo ili kuficha kutokuwepo.

8. Je, mfanyaazi anaweza kutumia likizo ya muda yenye malipo iwapo atakuwa mgonjwa au ana dalili zinazoweza kuwa na uhusiano na COVID-19?

Wafanyakazi wanaweza kutumia likizo ya ugonjwa yenye malipo kwa magonjwa ya mwili, majeraha au hali zingine za afya. Wanaeza pia kutumia likizo ya ugonjwa yenye malipo ili kuwatunza wanafamilia ambao wanaweza kuwa na magonjwa ya mwili, ajali majeraha, au hali zingine za afya.

9. Je, mfanyakazi anaweza kutumia likizo za ugonjwa yeneyee malipo iwapo daktari atapendekeza kwa sababu ya uwezekano wa maambukizi au dalili za COVID-19?

Ndio.

10. Je, mfanyakazi anaweza kutumia likizo ya ugonjwa yenye malipo iwapo anapata uaguzi wa tiba, utunzaji, matibabu, au utunzaji wa kuzuia ugonjwa au dalili zainazoweza kuwa na uhusiano na COVID-19?

Ndio.

11. Iwapo mwajiri atatoa likizo ya ugonjwa yenye malipo kama sehemu ya kutokuwa kazini na malipo (PTO), je, mfanyakazi anaweza kutumia likizo ya PTO kwa uhusiano na COVID-19?

Ndio.

12. Waajiri wanawezaje kutoa likizo ya ugonjwa yeneye malipo zaidi au kushughulikia malipo yaliopotea kwa sababu ya COVID-19 kwa wafanyakazi wao?

- Waajiri wanaweza kutoa likizo ya ugonjwa yenye malipo zaidi ya inayohitajika na sharia za likizo ya ugonjwa yenye malipo.
- Waajiri wanaweza kuwaruhusu waajiriwa wao kutumia likizo ya ugonjwa yenye malipo kwa madhumuni zaidi ya madhumuni ya chini zaidi yaliyoruhusiwa.
- Waajiri wanaweza kuchagua kuondoa kwa muda mahitaji ya thibitisho kwa wafanyakazi kutumia likizo ya ugonjwa kwa uhusiano na COVID-19.
- Waajiri wanawezatoa na kutekeleza sera mpya za kupeleka mbele likizo ya muda yenye malipo.
- Waajiri wanaweza kutoa malipo ya awali, mradi mapatano ya kulipa yanafikiana na kanuni za mkato mwafaka.
- Waajiri wanaweza kutoa sera za likizo ya kushirikiana. Wanaweza pia kuwakubalia wafanyakazi wao walio na salio ya likizo kutoa likizo hizo kwa wafanyakazi wenzao.